# UCHEZAJI WENYE UADILIFU WAKATI WA COVID-19

## KUWEKA JAMII YETU IKIWA YENYE AFYA NA SALAMA.

Afya na usalama wa watu ni muhimu. Ni muhimu zaidi ya mchezo au zawadi yoyote.

Ili watu wawe salama kutokana na COVID-19, tulifunga ofisi zetu katika maeneo ya Everett, Federal Way, Spokane, Vancouver na Yakima. Tulifunga pia maduka yetu katika viwanja vya ndege majengo yenye maduka, na ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia. Hatua hii ni ya muda mfupi tu.

Bado unaweza kucheza Lottery. Unaweza kununua tiketi kutoka kwa maduka na mashine za uuzaji. Unapaswa kununua tiketi wakati unapoenda kununua bidhaa zingine.

Washindi wanaweza kudai zawadi zao kwa njia salama. Washindi wa chini ya $600 wanaweza kupata zawadi yao katika maduka ambayo huuza tiketi za bahati nasibu. Kwa zawadi kuanzia $601 hadi $100,000, wachezaji wanaweza kutuma kwa barua tiketi za kushinda Lottery. Maelezo kuhusu jinsi ya kutuma tiketi kwa barua yapo hapo chini na kwenye tovuti yetu. Lazima utie saini tiketi zote kabla ya kuzituma kwa barua. Washindi walio na tiketi za $100,000 au zaidi wanapaswa kupiga simu kwa Makao makuu ya Lottery ili kupanga miadi ya kuja katika ofisi kuu mjini Olympia ili kupata zawadi.

Asante kwa kucheza Washington's Lottery. Kwa maelezo zaidi kuhusu COVID-19 katika Jimbo la Washington, tafadhali tembelea tovuti ya Idara ya Afya.

## MASWALI YANAYOULIZWA SANA YALISASISHWA 03.26.20

**Je, ni kwa nini mnafunga ofisi zenu?**
Washington's Lottery ilifunga ofisi zetu ili kuweka umma na wafanyakazi wetu salama. Tumefunga maduka yetu katika viwanja vya ndege na majengo yenye maduka, ofisi zote za maeneo ya (Everett, Federal Way, Spokane, Vancouver na Yakima), na ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia. Hatua hii ni ya muda mfupi tu.

**Je, hilo linamaanisha kwamba Washington's Lottery inafunga kabisa?**
Hapana. Bado tunafanya kazi na kuuza tiketi ya michezo yote. Michezo ya bahati nasibu inafanyika kama kawaida.

**Je, ofisi zote zitafungwa?**
Ofisi zote za kanda na maduka katika viwanja vya ndege na majengo yenye maduka zimefungwa. Ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia imefunguliwa kwa ajili ya huduma kupitia simu na barua pekee. Imefungwa kwa umma.

**Je, naweza kupata huduma gani?**
Ofisi za kanda hazitoi huduma wakati zimefungwa. Wachezaji wanaweza kutumia programu ya simu na tovuti ya Lottery ili kuangalia tiketi na kupata maduka ambayo yanauza tiketi za bahati nasibu. Baadhi ya maduka yamebadilisha saa zao za kazi, kwa hivyo wachezaji wanapaswa kuangalia saa za kazi za duka. Unapaswa kununua au kukomboa tiketi wakati tu wa kununua bidhaa kama vile chakula na mafuta. Maduka mengi bado yanauza na kuthibitisha tiketi, na hulipa tiketi za kushinda zenye thamani ya $600 au chini.

**Je, Lottery bado inacheza bahati nasibu?**
Ndiyo. Unaweza kupata zawadi kuu za sasa, nambari za kushinda, na tarehe za kucheza bahati nasibu kwenye programu ya simu au tovuti yetu.

**Je, kumekuwa na mabadiliko yoyote kwenye michezo au ratiba za kucheza bahati nasibu?**
Kwa wakati huu, hakuna mabadiliko.

**Je, ni kwa upesi kadri gani washindi wanaweza kukusanya zawadi zao?**
Maduka ya Lottery hulipa tiketi za kushinda zenye thamani ya $600 au chini. Maduka hulipa tiketi hizi mara moja, kama tu kawaida. Wachezaji wanaweza kudai tiketi za kushinda kuanzia $601 hadi $100,000 kwa kutuma barua. Washindi walio na tiketi za $100,000 au zaidi wanapaswa kupiga simu katika ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia kupanga miadi ya kufanya madai ya ana kwa ana. Washindi wana siku 180 za kudai zawadi. Washindi wanaweza kutia saini upande wa nyuma ya tiketi na kuhifadhi tiketi mahali salama hadi Ofisi zetu za Kanda zitakapofunguliwa.

**Je, ni nini kinatokea ikiwa mchezaji atashinda zawadi ambayo duka haliwezi kulipa?**
Ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia inafanya mchakato wa tiketi za kushinda zinazotumwa kwa barua. Washindi wanapaswa kutia saini upande wa nyuma ya tiketi na kufuata maagizo katika upande wa nyuma. Washindi wana siku 180 za kudai zawadi. Washindi wanaweza kutia saini upande wa nyuma na kuhifadhi tiketi yao mahali salama hadi Ofisi zetu za Kanda zitakapofunguliwa. Ikiwa mchezaji ana tiketi ya kushinda ya $100,000 au zaidi, anaweza kupiga simu katika ofisi kuu ya Lottery mjini Olympia ili kupanga miadi ya kufanya madai ya ana kwa ana.

**Je, maagizo ya kutuma barua ya tiketi ya kushinda ni gani?**
Washindi wanapaswa kufuata maagizo katika upande wa nyuma ya tiketi. Tiketi zinaweza kutumwa kwa barua kwa: Washington Lottery Headquarters, P.O. Box 43050, Olympia, WA 98504-3050. Lazima Lottery ipokee tiketi kabla ya tarehe ya mwisho ya siku 180. Haifai utume tiketi kwa barua katika siku ya tarehe ya mwisho.

**Je, ninapaswa kutuma barua ya tiketi yangu kupitia huduma iliyothibitishwa ya barua?**
Unaweza kutuma tiketi kupitia huduma iliyothibitishwa ya barua lakini sio lazima, Washindi lazima watie saini tiketi zao na wajaze upande wa nyuma kabla ya kutuma barua.

**Je, ninapaswa kupiga picha ya tiketi yangu ya kushinda kabla ya kuituma kwa barua?**
Unaweza kupiga picha tiketi yako ya kushinda ikiwa unataka. Lazima uwe na tiketi halisi ili ushinde zawadi.

**Ikiwa nitatuma tiketi yangu ya kushinda, je, zawadi zangu zitatumwa kwangu mara moja? Au ni lazima nisubiri hadi mfungue?**
Tunafanya mchakato wa tiketi za kushinda zinazotumwa kwa barua. Hilo halijabadilika.

**Je, kuna tarehe ya mwisho ya kukomboa tiketi ya kushinda?**
Ndiyo. Lottery lazima ipokee tiketi za kushinda ndani ya siku 180 baada ya tarehe ya kucheza bahati nasibu (kwa michezo ya kucheza bahati nasibu) au kufungwa kwa mchezo (kwa tiketi za *Kukwaruza*).

**Je, itakuwaje kama nina tiketi ya kushinda ambayo haijamaliza muda wa siku 180, lakini itakuwa imemaliza siku 180 au zaidi kabla mfungue barua?**
Lottery lazima ipokee tiketi za kushinda kabla ya tarehe ya mwisho. Wachezaji wengi hutumia huduma za barua zinazotumia usiku mmoja au za siku hiyo hiyo ikiwa tarehe ya mwisho inakaribia.

**Je, mnaongeza muda wa tarehe ya mwisho ya siku 180?**
Mabadiliko haya yatahitaji sheria za dharura. Kwa kuwa tunalipa tiketi za kushinda kupitia barua, hatukuongeza tarehe ya mwisho ya siku 180. Tunaweza kubadilisha uamuzi huu baadaye.

**Je, mnasafishaje Mashine za Uuzaji za Lottery?**
Maduka lazima yasafishe Mashine za Uuzaji za Lottery. Wafanyakazi wa Lottery pia husafisha Mashine za Uuzaji wakati wanabadilisha tiketi.

**Je, programu ya simu ya WA (Washington Lottery) itaendelea kufanya kazi na kusasishwa mara kwa mara?**
Ndiyo, programu bado inafanya kazi.

**Je, bado ninaweza kupata Pointi za Zawadi katika programu?**
Ndiyo, bado unaweza kupata na kukomboa Pointi za Zawadi.

**Je, bado ninaweza kuangalia tiketi za kushinda kwenye programu?**
Ndiyo, bado unaweza kuangalia tiketi ukitumia programu ya simu ya WA Lottery.